

HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA
MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA TIMU YA MENEJIMENTI CHA
TAREHE 21/10/2021

MAHURUDHURIO

1. Omary M Kangama - Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa
2. Zaina Ngala - Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi
3. Herbet Bilia - Mchumi wa Manispaa
4. Dr. Steven Ngwale - Mkuu wa Idara ya Mifungo na Uvuvi
5. Gerald Mwamhamila - Mkuu wa Idara ya Kilimo
6. Mwatumu Dossi - Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
7. Saadi Ishabailu - Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
8. Tupe Kayinga - Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
9. Charles Mwakalila - Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
10. Zabdiel Moshi - Mkuu wa Kitengo cha manunuzi
11. Charles Pengo - Afisa Tarafa Iringa Mjini
12. Dr. Jesca Leba - Mganga Mkuu wa Manispaa
13. Nicholous Mwakasungula - Mkuu wa Kitengo cha sheria
14. Gabriel Msunza - Mkuu wa kitengo cha uchaguzi
15. Godfrey Samali - Kaimu Mkaguzi wa ndani
16. Elizabeth Michael - Kaimu Mkuu wa Idara ya ujenzi

WASIOHUDHURIA

- 1) Priscus Shilima - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango Miji - kwa taarifa
- 2) Hamis Majaliwa - Afisa biashara - kwa taarifa

AGENDA: CMT/2021/2022/21 KUFUNGUA KIKAO

Kabla Mwenyekiti hajafungua kikao aliwakaribisha wajumbe kwa kuwaeleza kuwa kikao hicho ni maalumu ambacho hakiko katika ratiba ya vikao lakini amelazimika kukiitisha kutokana na umuhumi wa agenda inayokwenda kujadiliwa. Pia aliwataka wajumbe kuwa makini katika kutoa michango yao katika agenda hiyo muhimu baada ya maelezo hayo ya utangulizi alifungua kikao saa 3:15 asubuhi.

AGENDA: CMT/2021/2022/22 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO 19 KWA UTARATIBU WA FORCE ACCOUNT.

Mwenyekiti aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa imepokea mgao wa fedha kiasi cha Tshs 660,000,000/= toka serikali kuu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya UVIKO 19. Alieleza kuwa fedha hizo zina kusudiwa kutumika kutekeleza miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 33 katika shule za secondary za serikali 16 ambapo kwa mujibu wa maelekezo ya matumizi ya fedha hizo kila darasa limetengewa kiasi cha Tshs. 20,000,000/= kwa ajili ya ujenzi na samani. (Viti na Meza) kwa mchanganuo ufuatao:-


Mawelewele Sekondari, Tshs. 60,000,000/= (madarasa 3), Nduli sekondari Tshs. 40,000,000/= (madarasa 2), Mkwawa sekondari Tshs. 20,000,000/= (Darasa 1), Kigungawe Sekondari Tshs. 40,000,000/= (Madarasa 2), Mlandege Sekondari Tshs. 40,000,000/= (madarasa 2), Kwakilosa Sekondari Tshs. 20,000,000/= (darasa 1) Lugalo Sekondari Tshs. 40,000,000/= (madarasa 2), Ipogolo sekondari Tshs. 60,000,000/= (madarasa 3), Mtwivila sekondari Tshs. 20,000,000/= (Darasa 1), Iringa Sekondari Tshs. 20,000,000/= (Darasa 1), Tagamenda sekondari Tshs. 20,000,000/= (Darasa 1) Kreluu sekondari Tshs. 60,000,000/= (madarasa 3), Miyomboni sekondari Tshs. 20,000,000/= (Darasa 1), Kihesa sekondari Tshs. 40,000,000/= (Madarasa 2), Mvinjeni sekondari Tshs. 20,000,000/= (Darasa 1) Mlamke sekondari Ths. 20,000,000/= (Darasa 1).


Taarifa ilieleza zaidi kuwa fedha hizo tayari zimekwisha ingizwa katika account za shule husika na kuwa ujenzi unatarajiwa kufanyika kwa mujibu wa sheria za manunuzi kwa kuwatumia wakandarasi au utaraibu wa force account kulingana na mazingira ya kila Halmashauri. Aidha alieleza Zaidi kuwa utekelezaji wa mradi huo unatakiwa kufikia tamati ifikapo Novemba 30. Baada ya maelezo hayo alitoa nafasi kwa menejimenti kuchangia mawazo yao kuhusu namna bora ya kutekeleza miradi hiyo kwa kuzingatia viwango, sheria, kanuni na taratibu. Katika kujadili taarifa hiyo wajumbe walishauri utumike utaratibu wa force account kwa lengo la kupunguza gharama hasa ikizingatiwa kuwa kiasi cha Tshs.20,000,000/= kilichotengwa ni kidogo kwa kuzingatia gharama halisi za ujenzi. Mwisho Menejimenti kwa kauli moja iliridhia Kiasi cha Tshs. 660,000,000/= kilichotolewa na serikali kuu kitumike kujenga madarasa 33 katika shule za sekondari za serikali kwa utaraibu wa force account.

AGENDA: CMT/2021/2022/23 KUFUNGA KIKAO

Kabla Mwenyekiti hajafunga kikao aliwashukuru wajumbe wa timu ya menejimenti kwa michango yao ambayo imeweka msingi mzuri wa utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha alimtaka Mhandisi wa Manispaa kuhakikisha kuwa michanganuo ya gharama za ufundi na vifaa vinaandaliwa mapema na kuwasilishwa katika shule husika ili utekelezaji wa miradi hiyo uweze kuanza na kukamilika mapema kwa mujibu wa maelekezo ya serikali ambayo ni tarehe 30 mwezi Novemba baada ya maelezo hayo mwenyekiti alifunga kikao saa 6:10 Mchana

UMEDHIBITISHWA


.....
Gerald Mwachamila
Mwenyekiti


.....
Omary Mkangama
Katibu

Tarehe:.....*26-11-2021*.....